Learning by Ear 2011 – Mikinzano na utatuzi – “Palipo na wazee”
“Mizozo na utatuzi-palipo na wazee”
Kipindi cha 5: “Lazima tushinde”
AUTHOR: Chrispin Mwakideu
EDITOR: Andrea Schmidt, Aboubakary Liongo

## List of characters by scenes:

### SCENE ONE : MEETING BETWEEN MATONGE, SOMBA AND KERO

- **Matonge (m, 65)**
- **Somba (m, 55)**
- **Kero (f, 55)**

### SCENE TWO : BESIDE THE RIVER IN KIJANI VALLEY

- **Mitumba (m, 50)**
- **Waliani (m, 75)**
- **Masambo (m, 50)**
- **Mixed group (at least 4 ppl)**

### SCENE THREE: SOMBA AND KERO INSIDE THE ELEVATOR

- **Somba (m, 55)**
- **Kero (f, 55**

### SCENE FOUR: BESIDE THE RIVER AT KIJANI VALLEY

- **Mitumba (m, 50)**
- **Waliani (m, 75)**
- **Masambo (m, 50)**
- **Nina (f, 40)**
- **Mixed group (at least 4 ppl)**

Learning by Ear 2011 – Mikinzano na utatuzi – “Palipo na wazee”
“Mizozo na utatuzi-palipo na wazee”
Kipindi cha 5: “Lazima tushinde”
AUTHOR: Chrispin Mwakideu
EDITOR: Andrea Schmidt, Aboubakary Liongo

**Msimulizi**

**INTRO:**

Nawasalimu mabibi na mabwana. Karibuni tena katika Noa bongo! Jenga maisha yako. Hiki ni kipindi cha tano cha hadithi yetu, **“Palipo na wazee”.** Kipindi kilichotupungia mkono wa buriani, wakazi wa bonde la Kijani walikutana mtoni. Huko, wapiganaji wa Torube na Koroma, wakiongozwa na Masambo na Mitumba, walikuwa tayari wamefunga kibwebwe kuingia vitani. Lakini nia ya Mzee Waliani kubadilisha umwagikaji wa damu na kuwapatanisha itafaulu? Hebu tuyashuhudie hayo katika kipindi hiki cha tano, **“Lazima tushinde”.** Lakini kwanza, wacha niwapeleke katika mkutano unaofanyika kilomita mia moja kutoka hapa. Huu ulimuhusisha Rais Matonge, na swahiba zake wawili, Somba, mkuu wa majeshi na Kero, mkuu wa upelelezi.

**SCENE ONE: MEETING BETWEEN MATONGE, SOMBA AND KERO**

| 1. **SFX: PAPERS AND PAGES BEING SHUFFLED** |
|---|

| | |
|---|---|
| 2. **SOMBA:** | **(Insisting)** Rais Matonge, kufaulu kwako katika uchaguzi ujao mwakani kunategemea mawaidha yetu. |
| 3. **KERO:** | Mpaka kufikia sasa kura ya maoni inaonyesha bado uko nyuma ya Roselyn Tano kwa kura zaidi ya asilimia kumi! |
| 4. **SOMBA:** | Na kumbuka huyu ni mwanamke! Itakuwa aibu kubwa. |
| 5. **KERO:** | Suala la kuwa mwanamke kando, anatoka kabila la watorube . Watu hawa waliongoza nani isipokuwa |

ng’ombe zao malishoni.

**(Both Somba and Kero laugh sarcastically)**

6. **MATONGE:** **(Serious tone)** Nyamazeni Somba na Kero! Watorube pia ni wananchi wa taifa hili. Wengi walinipigia kura muhula uliopita. Swala la kujiuliza ni, kwanini wakati huu wamenipiga vita?

7. **SOMBA:** **(maliciously)** Walikupigia kwa sababu ulihonga kila familia na ng’ombe mmoja! Safari hii wanamtaka Roselyn kwa sababu ni mmoja wao. Ni mtorube!

8. **MATONGE:** Na wasia mzuri ambao nyinyi wawili munaweza kunipa , ni kuzusha mkinzano kati ya wa Torube na wana mgambo wa Kimbebe, hawa wezi wa ng’ombe waliohamia nchi jirani. Munafikiri ni sawa?

9. **KERO:** Sawa kabisa, bwana Rais. Makabila haya daima wanaibiana ng’ombe, wanapenda kupigana. Lakini sasa, kwa vile magaidi wa Kimbebe wana bunduki, maguruneti, mabomu na silaha nyengine, wa Torube hawawezi kuwashinda. Kama tutawapa silaha waTorube, vita baina yao vitazuka, watapigana miaka nenda miaka rudi.

10. **SOMBA:** Hilo litasababisha upigaji kura katika bonde la Kijani kutowezekana kwa sababu ni hatari kutoka majumbani.

11. **KERO:** Hilo ni thibitisho wazi kuwa utarudi tena kitini kwa mara yako ya ishirini baada ya kushinda kura bila kupingwa!

12. **MATONGE:** **(puzzled)** Bado sijawaelewa, Mnaniambia nimwage damu ya wananchi wangu mwenyewe?

13. **SOMBA:** **(stressing)** Tuanakwambia ufanye lolote ubaki katika utawala. Wewe tupe radhi zako, mengine utuwachie sisi.

14. **KERO:** Hivi tunavyozungumza, duru za kuaminika zasema kwamba watu wa Koroma na Torube hawako mbali kuzusha upya mzozo wao. Ni sisi tufikirie haraka tuwapatilize katika mvurugano wao.

15. **MATONGE:** Na akili yenu inawatuma kuwa huu mpango wenu utafaulu?

16. **SOMBA:** Bila wasiwasi wowote. Ikiwa hautafaulu, basi kuna mpango wa pili.

17. **MATONGE:** **(curious)** Mpango wa pili? Ambao ni?

18. **KERO:** Ndio maana ni mpango wa pili. Kwanza tujribu mpango huu. Unakubali bwana Rais?

19. **MATONGE:** Sijui. Unafikiria vipi Somba, wewe ndiye mkuu wa majeshi?

20. **SOMBA:** Ni lazima tuchukue hatua ya haraka ili kuondokana na zhali yoyote ya kutiliwa shaka . Lazima uonekane kama mzozo wa kawaida wa kabila hizo mbili.

21. **MATONGE:** **(Takes a deep breath)** Nipeni siku mbili nitawapa jibu.

22. **SOMBA:** **(urgency)** Hatuna muda huo wa siku mbili, Bwana. Kura zimeshafika.

23. **MATONGE:** Sawa. Basi siku moja!

**24. KERO:** **(protesting)** Lakini Mheshimiwa..

**25. MATONGE:** Mkutano umeisha!

**26. SFX: CHAIRS BEING PULLED AWAY INSTANTLY**

**27. MSIMULIZI:** Yale mkuu wa majeshi, Somba na mkuu wa upelelezi, Kero wanayopanga yanasumbuwa, na Rais Matonge aliwataka wampe muda wakufikiri. Ijapokuwa kule mashinani, alijuwa hana mtu mmoja aliye na imani naye. Ametumia mbinu na vitimbi vyote kubaki uongozini kwa miongo miwili, sasa inaonekana hatima yake imefika. Washauri hao wawili walipomuacha Rais na kuingia lifti kwenda zao walikuwa na shauku kubwa. Lakini kwanza, acha nikupeleke bonde la Kijani, kando ya mto, ambapo Waliani alipokuwa akinasihi amani na maridhiano kati ya wa Koroma na wa Torube.

**<u>SCENE TWO: BESIDE THE RIVER IN KIJANI VALLEY</u>**

**28. SFX: RIVER RUNNING SMOOTHLY**

**29. WALIANI:** Wakaazi wa bonde la Kijani. Masambo na Mitumba wameelezana bayana. Na wote wamekubali makosa yao. Si ni hivyo?

**30. MASAMBO:** Ndivyo, nitampa fidia Mitumba sawa na ile hasara niliyofanya shambani mwake.

**31. MITUMBA:** Nami naapa sitawazuia ng’ombe wako kunywa maji.

Nitalipa fidia ya maafa niliyotenda kwa kitendo hicho changu.

32. **(Gathering cheers wildly, ululating and whistling in joy)**

33. **WALIANI:** Ambavyo wawili hawa wamepatana, ni muhimu tueke ahadi mbele ya watu wote hawa, mbele ya babu zetu na Mungu mwenyewe. Kwamba hamutavamiana tena, na hamutaongoza makabila yenu vitani tena. Tunamchinja jogoo huyu kama ishara ya kuikata chuki iliyo dumu siku za nyuma. Na damu yake imwagwe kwenye mto huu.

34. **MITUMBA:** Nitamzuia kuku chini. Wewe endelea.

35. **MASAMBO:** Sawa, tafadhali nipeni kisu.

36. **MSIMULIZI:** Huku maandalizi ya maridhiano yakizidi kunoga, mkuu wamajeshi, Somba alikuwa tayari kwenye lifti, na rafiki yake, Kero akifuliza ili asimwache.

**<u>SCENE THREE: SOMBA AND KERO INSIDE THE ELEVATOR</u>**

37. **KERO:** **(Shouts)** Zuia lifti Somba! Naja ..

| 38. SFX: Person runs in elevator, LIFT DOORS OPEN |
|---|

39. **SOMBA:** Sikujua kuwa bado unaweza kukimbia!

40. **KERO:** (**Panting)** Mimi ni mkuu wa upelelezi. Watarajia nini? Nibonyezee ukumbi wa chini kabisa tafadhali.

| **41. SFX: LIFT DOOR CLOSES** |
|---|

**(ELEVATOR MUSIC PLAYING IN BACKGROUND)**

**42. SOMBA:** Wafikiria nini? Rais Matonge atakubali mpango wetu?

**43. KERO:** Itambidi, la sivyo Roselyn atamshinda.

**44. SOMBA:** Je asipowapa silaha wa Torube? Tutapindua serikali, iwapo atapoteza uchaguzi?

**45. KERO:** Unaogopa? Somba, wewe ndiye mkuu wa majeshi. Tutafanya lolote kuweka amani na kubaki uongozini.

**46. SOMBA:** Amani? Unazungumzia kuhusu amani ipi, kama tunapanga kupeana bunduki na risasi kwa wananchi?

**47. KERO:** **(Laughs)** Amani haiji ila kwa ncha ya upanga.

| **48. SFX: LIFT “PING” SOUND WHEN IT REACHES A STOP** |
|---|

**49. SOMBA:** Ninashuka hapa. Nijulishe lolote jipya, mkuu wa upelelezi.

| **50. SFX: LIFT DOOR OPENS** |
|---|

**51. KERO:** Hamna shaka, mkubwa.**(continues to laugh lightly)**

| **52. SFX: LIFT DOOR CLOSES** |
|---|

**53. MSIMULIZI:** Mizozo sio jambo jipya barani Afrika, imekuwepo tokea kaba ya enzi za ukoloni hadi katika kipindi cha mapambano ya kudai uhuru. Baada ya uhuru ikaja mizozo ya kuwania madaraka, rasilimali migawanyiko ya kidini, vita vya kikabila vilivyozagaa mpaka nchi jirani. Mizozo mingi kati ya hiyo ni matokeo ya mfumo wa kikoloni. Utawala wa kikoloni uliyavura maisha ya mwafrika ikiwa ni pamoja na utaratibu wa kutatua mizozo kwa njia ya maridhiano. Tukirudia riwaya yetu: Waliani amefikia kilele cha kupatanisha makabila haya mawili yaTorube na waKoroma. Baada ya kuchinja jogoo.

**SCENE FOUR: BESIDE THE RIVER AT KIJANI VALLEY**

**54. SFX: PEOPLE CROSS THROUGH A SHALLOW RIVER / WATER**

**55. WALIANI:** **(Prays)** Mungu wa mababu zetu, wewe uliyetuweka katika bonde hili. Wewe unayetupa mvua kwa msimu, ili tuweze kula tusife kwa njaa. Leo, makabila haya mawili yamekula kiapo. Yamekuwa familia moja kubwa. Tunaomba waheshimu umoja huu, yeyote atakayevunja, na wewe mvunje. Walikuja ili kuingia vitani. Sasa wanaondoka kwa amani.

**(Huge eruption of celebration and ululations from the mothers and men)**

**56. WALIANI:** Kama kuna mtu ana la kusema, aseme sasa au daima akae ukimya kwa amani . Kazi yangu ya leo imekwisha.

**57. MITUMBA:** Mzee Waliani, nilitoka nyumbani kwangu kwa ajili ya kuja vitani ili kuua na kuangamiza, nimebeba nyuta na mishale. Lakini sasa licha ya kupoteza mimea yangu yote, najihisi mwenye amani. Chuki yote imeondoka. Sihitaji tena hizi silaha. Nitazitupa motoni!

**(Again wild cheers, and applause from crowd gathered)**

**58. MASAMBO:** Mzee Waliani, ndugu na dada zangu. Leo, mababu zetu wanatabasamu kwa ajili yetu. Hata nami nitazitupa silaha zangu motoni. Nawashukuru akina mama waliogeuza akili zetu kuwa na hekima, sio ule uji uliokuwa umevunda vichwani mwetu.

**59. SFX: HUGE LAUGHTER**

**60. MASAMBO:** Nina ombi moja kabla ya kuondoka hapa mahala pamaridhiano. Mitumba, kwa niaba ya wavulana wangu wawili, Lawi na Gulu. Naomba mikono ya binti zako kwa nia ya ndoa timilifu.

**HITIMISHO:**

Ombi la mwisho lilimuingia vilivyo kila mtu, hata Mitumba. Jawabu lake litakuwa lipi? Ni kweli kuwa amani imepatikana na ndiyo mwisho wa mizozano? Ule mpango, wa kuwapa silaha waTorube na kuzua tafrani bondeni kati yao na waasi wa Kimbebe walio wezi wa mifugo, utafaulu? Kwa jawabu, sikiliza kipindi kijacho, cha mizozo na utatuzi. Ukitaka kusikiliza kipindi hiki au chengine kilichopita au kutupa maoni tembelea tovuti zetu www.dw.de/kiswahili

Mpaka tutakapokutana tena, jiepushe na siasa duni.